

SHULE YA UPILI YA GATITU
MTIHANI WA KATIKATI YA MUHULA WA KWANZA
KIDATO CHA TATU 2016

KISWAHILI

JINA.....DARASA.....NAMBARI.....

MATUMIZI YA LUGHA

a) Ainisha viwakilishi katika sentensi hii. (al. 2)

Wa kwanza alikabidhiwa vyote lakini akampa yule kimoja.

.....
.....
.....
.....

b) Onyesha mofimu katika ~~nao~~^{reno} hakijakataliwa. (al. 3)

.....
.....
.....
.....

c) Geuza sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (al. 2)

“Karibu Bakari, tafadhari kaa.” Juma akasema.

.....

d) Tambulisha aina za vielezi namna katika sentensi ifuatayo (al. 3)

(i) Wezi walipigwa barabara na umati wa watu

.....

(ii) Mnyama alifumwa mshale akaanguka chini pu

.....

.....

SHAIRI

SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI YANAYOFUATA

MJA SI MWEMA

a)Mja we inuka	inuka hima	twaa kalamu
Upate ya'ndika	na hati njema	hino nudhumu
Ipate someka	wenye kuisoma	waifahamu
Wapate yashika	na kuyapima	yaliyo humu
b)Andika anza	na sikawe	mkono wangu
Nami naanza	kisa chenye	cha mlimwengu
Livyonifanza	nao wajuwe	waja wezangu
Wapate jitunza	salama wawe	hawa ndu zangu
c)Mja sikudhani	sikudhaniya	tanizunguka
Nikamuamini	kafikiriya	hatageuka
Kumbe mwafulani	hakuzoweya	kuaminka
Nishabaini	ingawa baya	lishanifika
d)Menitenda kisa	kisa adhimu	mja mcheni
Mezinduka sasa	n'shafahamu	najuwa kwani
Ni yangu makosa	najilaumu	kumuamini
Si kuwa napasa	hata sehemu	kumthamini

e)Memjuwa mja	mja ni nduli	tahadharini
Mja si faraja	inda katili	hana imani
Muonapo mja	kaani mbali	mujitengeni
Asije akaja	kwani habali	kuhasirini

f)Mja hana haya	haya hazimo	mwake usoni
Mja kweli mbaya	hutimba shimo	ungiye ndani
Na ukisha ngiya	azome zomo	furaha gani
Mmoja kwa miya	ndiye hayumo	baya kundini

Maswali

1)Onyesha mambo yanayomkera msanii wa shairi hili. (al 4.)

.....

.....

.....

.....

.....

2)Fafanua muundo wa shairi hili al. 4)

.....

.....

.....

.....

.....

3)Shairi hili ni la bahari gani? (al. 3)

.....

.....

.....

.....

.....

